## HOTUBA YA WAZIRI WA KAZI NA AJIRA MHESHIMIWA GAUDENTIA M. KABAKA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio na Mapato ya Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu leo. Vile vile sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa walionipa ndani na nje ya Bunge katika kipindi chote cha Bunge hili la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nikishukuru Chama changu cha CCM, kwa imani kubwa kwangu katika kutekeleza Ilani ya Uchanguzi ya CCM ya mwaka 2010 nikiwa Mbunge na Waziri wa Kazi na Ajira.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sababu hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge hili la Kumi kabla halijavunjwa, niruhusu nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ***Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete*** kwa kuniteua kuwa mmoja wa washauri wake wakuu katika masuala yahusuyo Kazi na Ajira. Katika kipindi hiki cha miaka mitano nimejifunza mengi sana kutoka kwake na mimi nategemea kuwa nimetoa mchango uliotegemewa katika kumsaidia yeye kutimiza majukumu yake kama kiongozi mkuu wa nchi yetu, na pia katika kutimiza malengo tuliyojiwekea katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Pia, napenda nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dkt. Gharib Bilal** ambaye katika kipindi hiki cha miaka mitano, amekuwa mfano mkubwa kwangu wa uelewa, umahiri na uvumilivu katika uongozi. Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda** kwa uongozi wake na maelekezo yake mahiri katika utendaji wangu wa kazi wa siku hadi siku.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na maafisa wa Serikali wote ambao katika kipindi hiki wamenipa ushauri na ushirikiano mkubwa ulioniwezesha nitekeleze majukumu yangu kwa umakini kama Waziri wa Kazi na Ajira. Wote nawashkuru sana na nawaombea Mungu awabariki. Lakini kwa namna ya pekee kabisa napenda niwashukuru Mheshimiwa **Dkt Milton Makongoro,** Naibu Waziri wa Kazi

na Ajira, Katibu Mkuu wa Wizara yangu, **Ndugu Eric Shitindi;** Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara; Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambao nimefanya nao kazi kwa karibu sana na leo hii tumeifikisha Sekta ya Kazi na Ajira hapa tulipofika. Mwisho kabisa napenda niwashukuru sana Wasaidizi wangu katika Ofisi yangu kwa huduma, umakini na uvumilivu wao mkubwa. Wote hawa nawaombea Baraka za Mungu waendelee kuwa na afya tele.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kuwapongeza Viongozi wetu wa Chama na Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa mbalimbali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wana imani na Chama cha Mapinduzi, pamoja na Wabunge wake. Hivyo, nina amini kwamba wataendelea kuwapigia kura ili waendelee kuwawakilisha katika Awamu ijayo ya uongozi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti **Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga,** na Makamu Mwenyekiti **Mheshimiwa Albert Obama, Mbunge wa Jimbo la Manjovu** kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wote wa uhai wa Kamati hii na hususan wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016. Naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016 katika kikao chake kilichofanyika Dar es salaam tarehe 6 na 7 Mei, 2015. Kadhalika, ninaishukuru Kamati hii kwa kutembelea Taasisi na Miradi mbalimbali inayotekelezwa na Taasisi hizo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la Kigamboni na ujenzi wa nyumba za kisasa zinazojengwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika bajeti hii.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na jamaa wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki cha Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwarehemu. Aidha, kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii ambayo inasimamia Wizara yangu kwa kifo cha ghafla cha aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Marehemu Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Kifo hicho kimekuwa ni pigo kwa Kamati kwa kuwa Marehemu alikuwa nguzo imara katika Kamati hiyo. Nichukue fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu. Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi, **AMINA!**

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia (MDGs), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Awamu ya Pili, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Mikataba mbali mbali ya Kimataifa inayohusu masuala ya kazi na ajira na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Lengo la msingi la miongozo hiyo ni kuboresha maisha ya Wananchi; kudumisha amani; utulivu na umoja; kuimarisha utawala bora; kujenga uchumi madhubuti na endelevu; kuboresha afya na kutunza mazingira. Wizara yangu imetekeleza miongozo hiyo kwa kuimarisha viwango vya kazi, kuhakikisha kuna mazingira yanayokidhi afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi, kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha ushirikishwaji wa wafanyakazi na kukuza ajira nchini. Mafanikio yaliyopatikana yamewezesha kuendelea kuwa na utulivu katika sekta ya kazi, hali ambayo imesaidia kukua kwa uchumi na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje hivyo kukuza ajira kwa makundi mbali mbali ya wananchi katika nchi yetu na kuwapunguzia umasikini wa kipato.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijaanza kutoa taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa **Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.)** na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa **Dkt. Mary Nagu** Mbunge wa Jimbo la Hanang kwa hotuba zao nzuri ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, sehemu ya pili ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 na sehemu ya tatu ni Malengo ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo hayo.

## B. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2010 – 2015)

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imetekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, hususan **Ibara ya 78** vifungu (b na c), **Ibara ya 79** vifungu (a-b) na **Ibara ya 81** vifungu (i-j) kuhusu Ajira, **Ibara ya 80** vifungu (a-c) kuhusu Kazi na **Ibara 82** vifungu (a-e) kuhusu Hifadhi ya Jamii kama ifuatavyo:

*Ibara ya 78, kifungu (b);*

**Kufanya utafiti wa kina wenye lengo la kuandaa mpango wa muda mrefu utakaowashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea.**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimballi ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya uchambuzi wa hali halisi ya soko la ajira kupitia Utafiti wa Nguvu Kazi (*Intergrated Labour Force Survey*). Pia, Wizara imefanya mashauriano na wadau wa sekta ya ajira ikiwemo Wakuu wa Mikoa, Sekta Binafsi, Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kubaini changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana na namna ya kukabiliana nazo. Mashauriano haya yamebaini kuwa changamoto kubwa kwa sasa zinazowakabili vijana katika kujiajiri ni pamoja na ukosefu wa ujuzi, ukosefu wa miundombinu ya kuwezesha kujiajiri, ukosefu wa mitaji pamoja na mtazamo hasi kuhusu kujiajiri miongoni mwa vijana. Uchambuzi huu umewezesha Wizara kuandaa Programu ya Kukuza Ujuzi pamoja na Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana. Programu hizo zinalenga kuwajengea uwezo Vijana wa kuajiriwa na kujiajiri katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Utekelezaji wa Programu hizo zitaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/16 na zinahusisha wadau mbalimbali.

*Ibara ya 78, kifungu (c);*

**Kuimarisha Shirika la Tija la Taifa ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa uchumi nchini.**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha Shirika la Tija la taifa Wizara imefanya uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi na kuongeza idadi ya watumishi ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi zilizokaimiwa kwa muda mrefu. Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi umezingatia uzoefu na ujuzi wao katika masuala ya kiuchumi. Aidha, katika kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2011 hadi 2015, Shirika limetoa mafunzo 346 ya kuboresha tija kwa taasisi mbali mbali sawa na asilimia 87 ya lengo.

*Ibara ya 79, kifungu (a);*

**Serikali kuibua Mpango Kabambe wa kuwawezesha kiuchumi vijana wasomi walio tayari kujituma kwa kujiajiri ili watumie nguvu na maarifa waliyonayo katika kilimo, ufugaji na uvuvi wa kisasa.**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Programu ya kukuza ajira kwa vijana ya miaka mitatu itakayowawezesha kutoa fursa za ajira kwa vijana 840,000. Programu hii imelenga kuwajengea vijana uwezo na ujuzi wa stadi mbalimbali za

kazi na ujasiriamali; kuwawezesha kupata mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali; na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kushiriki katika kukuza ajira kwa vijana. Miongoni mwa wadau wanaoshiriki katika ukuzaji ajira ni pamoja na Umoja wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUGECO), Shirika la TechnoServe kupitia Mradi wa kuwezesha vijana kujiajiri katika kilimo mkoani Mbeya; Baraza la Taifa Uwezeshaji kupitia "**Programu ya Kijana Jiajiri**"; Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana na wadau wa Utalii na Chuo cha Taifa cha Utalii kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi katika sekta ya hoteli pia kwa kushirikiana na VETA kwa kutekeleza programu ya kutambua ujuzi uliopatikana kupitia mfumo wa elimu usio rasmi. Miradi iliyotekelezwa imelenga kutoa mafunzo ya ujasiriamali na namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara ikiwemo mradi wa Kazi Nje Nje ambapo mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa vijana 35,325; miongoni mwao vijana **11,825** ni wahitimu wa elimu ya juu. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya ajira **1,929,938** zilizalishwa nchini tofauti na lengo la kuzalisha ajira milioni moja katika kipindi hicho cha miaka mitano. Idadi hii inajumuisha ajira Kilimo ajira **417,531**; Elimu ajira **144,764**; Afya ajira **29,444**; Ujenzi wa Miundombinu ajira **200,484**; Nishati ajira **1,479**; Miradi ya Kijamii ajira **102,948;** Sekta nyingine Serikalini ajira **15,240.** Jumla ya ajira zilizozaliwa katika Sekta binafsi ni **1,018,048** kwa mchanganuo ufuatao: Mawasiliano ajira **184,030;** Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira **26,098** na Miradi ya uwekezaji kupitia kituo cha TIC ni **325,622;** uwekezaji katika vituo vya EPZ **67,646 na** sekta nyingine za uwekezaji ni **414,652 (Jedwali Na 1)**.

*Ibara ya 80, kifungu (a);*

**Kuendelea kuboresha mishahara ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wa nchi utakavyoruhusu.**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mishahara, Serikali iliunda Bodi za kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kutoka Bodi 8 zilizokuwepo mwaka 2010 hadi Bodi 12 mwaka 2011. Kutokana na mapendekezo ya Bodi hizo, tangu mwaka 2010 hadi sasa kima cha chini cha mshahara katika Sekta Binafsi kimeongezwa mara mbili, mwaka 2010 na 2013. Nyongeza hizo zimezingatia vigezo vya kiuchumi na tija katika kila sekta. Aidha nyongeza ya mwaka 2013 ilikuwa kati ya asilimia 21 hadi 65 ya viwango vya mishahara vya mwaka 2010.

*Ibara ya 80, kifungu (b);*

**Kuimarisha na kufanya kaguzi za kazi, ikiwa ni pamoja na masuala ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya kaguzi **220,350** zimefanyika ikiwa ni wastani wa kaguzi **40,000** kwa mwaka. Lengo

la kaguzi hizo ni kuhakikisha waajiri wanafuata Sheria za Kazi ipasavyo. Jumla ya kaguzi za kawaida **26,412** na kaguzi maalum **53,807** kuhusiana na afya na usalama mahala pa kazi zimefanyika. Wafanyakazi **136,076** walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari za kiafya zitokanazo na maeneo wanayofanyia kazi. Pia, Serikali imeendelea kuimarisha Ofisi za Kazi za Mikoa kwa kuziongezea bajeti na idadi ya watumishi kwa lengo la kuziwezesha kusimamia kikamilifu Sheria na viwango vya kazi katika maeneo yao. Katika mwaka 2014/2015 Wizara imeajiri watumishi **24** ili kuimarisha ukaguzi wa viwango vya kazi nchini.

*Ibara ya 80, kifungu (c);*

**Kusuluhisha na kuamua kwa wakati migogoro yote ya kikazi na kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi**

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2010 hadi mwezi Aprili, 2015 jumla ya migogoro **10,281** imesuluhishwa na jumla ya migogoro **6,057** imeamuliwa na Tume ya Usuhishi na Uamuzi (CMA). Katika kipindi hicho muda wa kusikiliza na kusuluhisha umepungua kutoka siku **30** hadi siku **12** na muda wa kusikiliza na kuamua umepungua kutoka siku **90** hadi siku **85.** Pia, elimu kwa umma kuhusu Sheria za Kazi ilitolewa kwa wafanyakazi wapatao **1,908,000** na waajiri **6,890**. Hadi sasa jumla ya Mabaraza ya Wafanyakazi **265** yameundwa katika Taasisi za Umma ikiwa ni sawa na asilimia **86.6** ya lengo;

Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za wafanyakazi na waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za vyama vya wafanyakazi na waajiri. Katika kipindi cha 2010 hadi 2015, jumla ya vyama **7** vya wafanyakazi vilisajiliwa na shirikisho moja la vyama vya wafanyakazi liliundwa na kusajiliwa. Lengo ni kuongeza na kuboresha wigo wa ushiriki wa wafanyakazi, majadiliano na utetezi wa haki za wafanyakazi na waajiri katika sehemu za kazi. Jumla ya vyama vya wafanyakazi vilivyosajiliwa nchini hadi sasa ni **31**, ikilinganishwa na vyama **24** vilivyokuwepo mwaka 2009. Hadi sasa tuna vyama **viwili** vya waajiri (ATE na TAACIME), Mashirikisho mawili ya vyama vya wafanyakazi (TUCTA na FEATU) na Shirikisho moja la vyama vya Waajiri wa Afrika Mashariki (EAEO) na Shirikisho la Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi wa Afrika Mashariki –EATUC. **(Rejea Kiambatisho Na. 2)**

*Ibara ya 81, kifungu (i);*

**Serikali kuandaa mafunzo maalum kwa vijana ya kupenda kufanya kazi na kuwa waadilifu ili waweze kuajirika**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imehuisha elimu ya kujitegemea katika mfumo wa elimu na mafunzo, pamoja na kurejesha mfumo wa vijana kupitia katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Aidha, Serikali imepitisha Sera ya Taifa

ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo inazingatia utengenezaji wa mitaala inayozingatia mahitaji ya soko la ajira.  Pia, kupitia Programu ya kukuza Ajira kwa Vijana ambayo ilianzishwa mwaka 2013; mafunzo maalum ya kubadili fikra kwa vijana (change of mind set) ni sehemu mojawapo ya mtaala wa mafunzo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani na Wadau wengine tangu mwezi Julai 2014, zimeandaa Programu ya Mafunzo kwa vitendo kazini (*Apprenticeship)* kwa wahitimu wa vyuo ambao hawajaajiriwa ili kuwawezesha kupata stadi na sifa za kuajiriwa na kupenda kufanya kazi. Programu imeanza na imefanyiwa majaribio katika sekta ya utalii.

*Ibara ya 81, kifungu (j);*

**Serikali kusimamia kikamilifu Sheria ya Ajira ya Wageni**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imepitisha Sheria ya Ajira kwa wageni ya mwaka 2014 katika Bunge la 19 mwezi Machi, 2015. Sheria hiyo imeweka mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni.

*Ibara ya 82, kifungu (a);*

**Kufanya tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kurekebisha viwango vya mafao vinayotoa ili visipishane mno.**

**20.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha 2010 tathmini ya mifuko ya hifadhi ya jamii ilifanyika ambapo matokea ya tathmin hiyo yalionesha kwamba hali ya mifuko ni nzuri isipokuwa Mfuko wa PSPF ambao hali yake ya kifedha si ya kuridhisha kutokana na deni la Serikali linalotokana na malipo ya pensheni kwa wastaafu ambao hawakuchangia kabla ya Julai 1999 (Pre 99). Kutokana na matokeo ya tathmin hiyo, Serikali imeanza kulipa deni la PSPF kwa awamu. Aidha, kuanzia Julai 2014, Serikali imerekebisha kanuni za kukokotoa mafao ya pensheni, hatua ambayo imesaidia kuondoa tofauti ya malipo ya mafao ya pensheni kwa wanachama katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mabadiliko haya ambayo yameambatana na vikokotoo vipya, yameboresha mafao ya kila mwezi ya pensheni kutoka 67% kwenda 72.5%. vile vile kanuni hizi zinathaminisha pensheni (indexation) na hivyo kuboresha pensheni kwa kiwango kikubwa.

*Ibara ya 82, kifungu (b);*

**Kuanzisha na kuimarisha Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

**21. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) nchini mwaka 2010, kwa lengo la kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Aidha, Serikali ilirekebisha Sheria ya Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kupitia Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 ili kuipa SSRA mamlaka ya kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine imeimarisha Mamlaka na kuboresha utendaji wa Mifuko. Hadi kufikia Juni,Machi, 2015 SSRA imetoa jumla ya miongozo 11 ya kuongoza na kuimarisha Sekta. Miongozo na kanuni hizo ni;

i) Mwongozo wa Uendeshaji wa Bodi za Wadhamini wa Mifuko (2012)
ii) Mwongozo wa Utunzaji wa Kumbukumbu na Takwimu (Data Management Guidelines) 2012
iii) Mwongozo wa Utangamano wa Mifumo ya TEHAMA (2014)
iv) Mwongozo wa Usalama wa TEHAMA (Security of Electronic Information)
v) Mwongozo wa Majumuisho ya Vipindi Vya Uchangiaji (2013/2014)
vi) Miongozo ya Tathmini (Actuarial guidelines)
vii) Miongozo ya uwekezaji (Investment guidelines) ya 2012
viii) Mwongozo wa Uandikishaji wanachama wa 2013
ix) Mwongozo wa Uendeshaji wa Mikutano ya kila mwaka ya wanachama (2014)
x) Mwongozo wa Uwasilishwaji wa Taarifa za Mwaka (2014)
xi) Kanuni ya Kuhuisha Mafao ya pensheni (2014)

*Ibara ya 82, kifungu (c);*

**Kuchukua hatua za makusudi za kupanua wigo wa kinga ya jamii ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma ya hifadhi ya jamii**

**22. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia kifungu cha 30 cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2008, kwa kuruhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuandikisha wanachama kutoka sekta yoyote kwa kuzingatia Sheria na Mwongozo wa Uandikishaji Wanachama wa mwaka 2013. Aidha, Sheria hiyo pia imetoa fursa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii kusajili wanachama kutoka katika sekta isiyo rasmi, ambapo hadi sasa wanachama wapatao 40,000 wamejiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pia, Serikali katika jitihada za kupanua wigo wa huduma ya hifadhi ya jamii kupitia Sheria Na. 8 ya mwaka 2013, imebadili GEPF kutoka Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi na kuwa Mfuko wa Pensheni ili kuwezesha mwananchi yoyote kujiunga na kufaidi mafao ya kila mwenzi ya uzeeni. Aidha, wanachama katika sekta ya Hifadhi ya Jamii wameongezeka mara mbili kutoka **900,000** mwaka 2010 hadi kufikia zaidi ya **2,000,000** mwaka 2015; Rasilimali za Mifuko ya hifadhi ya Jamii zimeongezeka kutoka **trillion 1.3** mwaka 2005 hadi kufikia **trilioni 8** mwaka 2015; Mafao ya wanachama walionufaika imekua kutoka shilingi **bilioni 131** mwaka 2005 hadi kufikia **shilingi trilioni 1.3** mwaka 2015; Wastaafu (pensioners) wameongezeka toka 24,000 mwaka 2005 kufikia takribani 100,000 mwaka 2015.

Kwa ujumla idadi ya watu wanaonufaika na huduma za hifadhi ya jamii imefikia watu **milioni 6.5** mwaka 2015 kutoka watu **690,000** mwaka 2005. Vile vile, mwaka 2014/2015 Serikali imeanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaougua au kuumia kazini. Mfuko huu utaanza kutekeleza wajibu wake katika mwaka 2015/2016.

*Ibara ya 82, kifungu (d);*

**Kuelimisha jamii ya wafanyakazi na waajiri juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa maendeleo ya wafanyakazi na ya nchi kwa ujumla.**

**23. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kupitia SSRA na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kutoa elimu ya Hifadhi ya Jamii kupitia vyombo mbalimbali vikiwemo semina, warsha, radio, magazeti, mitandao ya kijamii, digitali, tovuti ya Mamlaka, machapisho, vipeperushi na runinga. Watu waliofikiwa ni zaidi ya **5,450,000**. Aidha, Mifuko yote imekuwa ikifanya mikutano ya mwaka ya wanachama, ambapo wanachama husika wamekuwa wakipatiwa taarifa mbalimbali zinazohusu uendeshwaji wa Mifuko. SSRA pia imetoa elimu kwa makundi maalum, wakiwemo vyama vya wafanyakazi, waajiri, waheshimiwa wabunge, wajasiriamali, wanafunzi wa vyuo, mabaraza ya wafanyakazi wa taasisi mbalimbali, waandishi na wahariri, wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi

*Ibara ya 82, kifungu (e);*

**Kuendelea kutumia uwezo wa kifedha uliopo katika kila shirika la hifadhi ya jamii, kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya nchi.**

**24. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kubuni huduma na mafao mbalimbali kwa wanachama wake kwa lengo la kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii, kuongeza ajira na kudumisha utulivu wa kisiasa nchini. Mifuko hiyo iliendelea kuwekeza rasilimali katika maeneo yanayolenga kujenga uchumi wa kisasa ikiwa ni pamoja na elimu, afya, makazi, michezo, miundombinu, mapinduzi ya viwanda na kilimo. Mwongozo wa Kusimamia Uwekezaji wa mwaka 2012 umeweka vipaumbele kwenye uwekezaji wa miradi mnyambuka (multiplier effect) kwa kuzingatia hadhari na kipato (risk and return). Aidha uwekezaji umeongezeka kutoka **shilingi trilioni 1.6** mwaka 2006 hadi kufikia **shilingi trilioni 7** mwaka 2015. Hili ni ongezeko la asilimia 250. Vile vile, mikopo ipatayo **shilingi bilioni 130** imetolewa kwa wanachama wa vikundi mbalimbali.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KAZI KWA MWAKA 2014/2015

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kuhusu viwango vya kazi, usawa na ajira ya staha, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji ukuzaji wa tija mahali pa kazi na hifadhi ya jamii nchini. Katika mwaka 2014/2015 tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

### I. WIZARA YA KAZI NA AJIRA

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza majukumu yake ya kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi, uboreshaji wa hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 jumla ya **shilingi 9,606,000** zilikadiriwa kukusanywa ikiwa ni mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya Wizara. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **shilingi 3,120,000** sawa na **asilimia 33** ya makadirio.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara (**Fungu 65),** ilikasimiwa jumla ya **Shilingi 17,654,394,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,815,289,000** sawa na **asilimia 33** zilitengwa kwa ajili ya kulipa mshahara wa Watumishi (PE), **Shilingi 8,914,105,000** sawa na **asilimia 50** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na **Shilingi 2,925,000,000** fedha za Maendeleo sawa na **asilimia 17**.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, **Shilingi 4,744,071,997** sawa na **asilimia 82** ya fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na **shilingi 2,692,134,371** sawa na **asilimia 30** ya fedha za Matumizi mengine (OC ) zilitolewa na kutumika na Wizara. Hakuna fedha za Bajeti ya Miradi ya Maendeleo zimetolewa mpaka sasa**.**

#### Usimamizi wa Kazi na Huduma za Ukaguzi

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** *Wizara* imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Utekelezaji umefanyika kwa kukagua sehemu za kazi, kutoa elimu ya Sheria za kazi kwa wafanyakazi na waajiri na kuchukua hatua za kisheria kwa wasiozingatia Sheria za kazi. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na wafanyakazi kupitia vyama vyao na

kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza mahusiano mema baina ya waajiri na wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kaguzi za kazi **1,754** zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi. Kaguzi hizo zililenga katika kuangalia utekelezaji wa viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi. Kupitia kaguzi hizo, waajiri **244** walipewa amri tekelezi *(compliance orders*) baada ya kubainika kuwa wanakiuka Sheria na waajiri **9** wamefikishwa mahakamani kwa kushindwa kutekeleza amri zilizotolewa. Vile vile, maafisa Kazi **11** wamejengewa uwezo wa namna ya kufanya ukaguzi wa viwango vya kazi kwa wafanyakazi wa majumbani.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa Wafanyakazi **3,536** na Waajiri **673** wa sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Hoteli, Ulinzi binafsi na Usafirishaji. Wizara pia, imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa na kikanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika - SADC, Umoja wa Afrika na Shirika la Kazi la Kimataifa) iliyohusu masuala mbalimbali ya kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa sheria za kazi, kuimarisha jitihada za kukabiliana na utumikishwaji wa watoto ikiwa ni pamoja na kufanyika kongamano la kutokomeza ajira mbaya ya mtoto katika sekta ya kilimo na usafirishaji wa binadamu.

**Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuandaa mfumo sahihi wa kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika kupanga kima cha chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi. Kwa sasa mfumo unaotumika katika upangaji wa Kima cha Chini cha Mshahara katika sekta binafsi ni kutokana na ushauri unaotolewa na Bodi za kisekta. Utaratibu huu umesababisha malalamiko kutoka kwa waajiri na wafanyakazi kwa kutozingatiwa kwa uwiano sahihi wa vigezo vya kiuchumi na tija katika kupanga kima hicho kwa kila sekta. Katika kuboresha mfumo huo, Wizara iliunda Kikosi Kazi cha Utatu cha wajumbe kutoka Serikalini, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri ambacho kimependekeza mfumo sahihi wa kuwa na Bodi Moja ya kupendekeza Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha wafanyakazi na waajiri kujadiliana kwa pamoja katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Katika kipindi hiki jumla ya Mikataba ya Hali Bora **67** ilisainiwa na kusajiliwa na Kamishna wa Kazi. Mikataba hiyo inahusisha sekta za Viwanda, Maji, Biashara pamoja na Hoteli.

**Hifadhi ya Jamii**

**35. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2015 Wizara kwa kushirikiana na SSRA imetoa elimu hifadhi ya jamii kwa watu **517,951** na kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) na Makampuni binafsi. Aidha, Mamlaka imeandaa na kutekeleza mkakati wa elimu kwa umma. Elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa katika vipindi 173 vya runinga na redio na kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na magazeti, mikutano na waandishi wa habari na ushiriki katika maonesho. Pia, zilifanyika tafiti **tatu (3)** zenye lengo la kupanua wigo wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Hizi zilijumuisha huduma zisizo rasmi za bima ya afya (social health insurance) na misaada ya kijamii (social assistance). Vile vile Serikali, imetoa Kanuni mpya ya kuwianisha mafao ya pensheni (benefits harmonization rule) iliyoanza kutumika tarehe 01 Julai, 2014.

**Fidia kwa Wafanyakazi (The Workers Compensation Fund)**

**36. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2014/2015 imekamilisha taratibu muhimu za kuanza kuendesha Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi. Mfuko huo unaanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 74(1) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*). Hatua hizo muhimu zilizotekelezwa katika kuanzisha mfuko huo ni pamoja na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Kanuni kuhusu viwango vya michango kwa makundi ya Waajiri kwa mwaka 2015/16 ambapo Serikali itachangia **asilimia 0.5** ya mshahara wa kila mtumishi kila mwezi na Taasisi Binafsi watachangia **asilimia 1** ya mshahara wa kila Mfanyakazi kila mwezi. Hatua nyingine iliyotekelezwa katika kuanzisha Mfuko huo wa Fidia ni kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko.

**Vita dhidi ya Ajira Mbaya kwa Mtoto**

**37. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la *International Rescue Committee*-WEKEZA imeendelea kupambana na utumikishwaji wa watoto katika mikoa ya Tanga na Kigoma. Kupitia Mradi huu, jumla ya watoto **8,538** wamezuiwa kuingia kwenye utumikishwaji na kupatiwa shughuli mbadala ikiwa ni pamoja na elimu ya shule ya msingi kwa watoto **4,619,** elimu ya Sekondari kwa watoto **1,884** na elimu kwa watoto **2,035**waliokosa elimu ya msingi**.** Aidha, kupitia Mradi huu, elimu ya sheria za kazi hususani katika masuala yanayohusu katazo la utumikishwaji wa mtoto ilitolewa kwa Walimu **411,** Wajumbe wa Kamati za shule **513,** Wajumbe wa VICOBA **2,398,** Vijana **4,738** wenye umri kati ya miaka 15 hadi 17 na Maafisa wa Serikali za Mitaa **3,042.**

**Ushirikishwaji wa Wafanyakazi**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Hatua hii imesaidia sana kuboresha mahusiano na kuwepo hali ya utulivu mahali pa kazi. Aidha, kutokana na elimu iliyotolewa Wizara ilitatua jumla ya migomo 9 iliyopokelewa kutoka kwa waajiri wa sekta za Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji walio katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Mwanza, Musoma na Kigoma.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikishaji wa wafanyakazi nchini, Wizara iliratibu kikao kimoja cha viongozi wa vyama vya Wafanyakazi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali kuhusiana na hali na maslahi ya wafanyakazi nchini.

**Ukuzaji wa Ajira Nchini**

**40.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha awadau mbalimbali kushiriki katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 pamoja na kuratibu shughuli husika. Katika mwaka 2014/2015, wadau walioshiriki katika kuandaa na kutekeleza programu za kukuza ajira ni pamoja na: TechnoServe kupitia Mradi wa kuwezesha vijana kujiajiri katika kilimo mkoani Mbeya; Baraza la Taifa Uwezeshaji kupitia “Programu ya Kijana Jiajiri” inayowezesha vijana kujiajiri; Shirika ka Kazi Duniani kwa kushirikiana na wadau wa Utalii na Chuo cha Taifa cha Utalii kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi katika sekta ya hotel; Shirika ka Kazi Duniani kwa kushirikiana na VETA kwa kutekeleza programu ya kutambua ujuzi ulipatikana kupitia mfumo wa elimu usio rasmi. Aidha, katika kuweka msukumo zaidi kwa Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuendeleza juhudi za kukuza ajira hasa kwa vijana katika ngazi za Wilaya na Mikoa, wizara iliandaa Kongamano la Wakuu wa Mikoa lililofanyika mwezi Novemba, 2014 kuhusu ukuzaji wa ajira nchini. Kupitia Kongamano hilo, Wizara imewekeana Mkataba (*Memorandum of Understanding*) na Wakuu wa Mikoa la kukuza ajira kwa vijana na kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri. Pia, Wizara imeratibu ushiriki wa Wajasiriamali wadogo 120 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwenye Maonesho ya 14 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 1 hadi 7 mwezi Desemba, 2014 mjini Kigali nchini Rwanda.

**Kuimarisha ukusanyaji taarifa na takwimu za ajira**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, **Wizara** imeendelea kuimarisha mfumo wa taarifa za soko la ajira nchini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya ajira **574, 040** zilizalishwa katika sekta za: Kilimo ajira **154,560**; Elimu ajira **36,071**; Afya ajira **3,452**; Ujenzi wa Miundombinu ajira **107,527**; Nishati ajira **378**; Miradi ya ya Kijamii ajira **9,455;** Sekta nyingine

Serikalini ajira **5,274.** Jumla ya ajira zilizozalishwa katika Sekta binafsi ni **257,322** kwa mchanganuo ufuatao: Mawasiliano ajira **6,809;** Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira **6,524** na Miradi ya uwekezaji kupitia kituo cha TIC ni **34,164;** uwekezaji katika vituo vya EPZ **16,911 na** sekta nyingine za uwekezaji ni **192, 895 (Kiambatisho Na. 3)**

**Huduma za Ajira**

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia Kanuni za huduma za ajira zinazotolewa na Wakala Binafsi, Wizara imefanya uchambuzi wa maombi ya usajili wa Mawakala Binafsi **126** wa Huduma za Ajira ambapo kati yao Mawakala **96** walipewa usajili wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 13/03/2015 hadi 12/03/2016.

**Uratibu wa Ajira za Wageni**

***43. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia ajira za wageni nchini kwa lengo la kuhakikisha ajira hizo ni kwa manufaa ya nchi na pia kulinda ajira za Watanzania; Wizara imeratibu utungaji wa Sheria ya Ajira za Wageni kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni. Sheria hiyo imeweka mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni kwa kuzingatia ujuzi adimu nchini.

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi **9,271** ya vibali vya ajira za wageni vya Daraja B. Kati ya maombi hayo, maombi **8,890** (96%) yalipendekezwa kupewa vibali na maombi **381** (4%) yalikataliwa (**Kiambatisho Na. 4)**

**Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka kazi zifuatazo zimetekelezwa:

i) Kusajili Chama kimoja cha wafanyakazi cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA);

ii) Kukagua taarifa za hesabu za vyama 5 vya wafanyakazi;

iii) Kukagua vyama 8 katika ngazi ya taifa katika kuhakikisha vyama hivyo vinatimiza masharti ya usajili kulingana na matakwa ya Sheria; na

iv) Kutoa elimu juu ya uhuru wa kujumuika na kujiunga na vyama vya wafanyakazi na waajiri na kuwakumbusha viongozi na wananchama wa

vyama kuheshimu Katiba za vyama vyao kuepuka migogoro. Wafanyakazi 102 na wajumbe 30 kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) walipatiwa elimu hiyo.

**Kujenga Uwezo wa Wizara**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2014/2015 tumetekeleza yafuatayo katika kujenga uwezo wa Wizara:-

i) Kuajiri watumishi 21 kupitia Tume ya Ajira Serikalini ambao ni Maafisa Kazi Daraja la II na tayari wameshapangiwa vituo vya kazi mikoani;

ii) Watumishi 40 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watumishi 4 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Aidha, jumla ya watumishi 100 wamepatiwa mafunzo ya Maadili katika Utumishi wa Umma; na

iii) Kusimamia zoezi la OPRAS kwa watumishi 262 wa Wizara kulingana na mwongozo wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

## II. TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi **saba** za umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), Shirika la Tija la Taifa (NIP), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Mfuko wa Fidia ya Wafanyakazi. Mapitio ya utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2014/2015 kupitia taasisi hizi ni kama ifuatavyo:

**Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi una wajibu wa kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kusajili sehemu za kazi, kufanya ukaguzi na kupima afya za wafanyakazi. Wizara katika mwaka 2014/2015 kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imetekeleza kazi zifuatazo;

i) Kufanya ukaguzi **4,862** wa kawaida (*General Workplace inspection*) na ukaguzi maalum **18,236** sawa na asilimia **151.9** ya ukaguzi **12,000** uliopangwa kufanyika. Ukaguzi huu ulifanywa kwenye maeneo ya Umeme, Mitambo ya kuzalisha mvuke (boilers), Mitungi ya hewa na Mvuke, Zana za kunyanyulia vitu vizito na Vipimo vya mazingira.Aidha wafanyakazi 45,721

walipimwa afya zao sawa na asilimia **101.6** ya lengo la kuwapima wafanyakazi **45,000**

ii) Kukamilisha taratibu za kupendekeza kuridhia mikataba 6 ya Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Mikataba hiyo ni Mkataba Na.155 (Occupational Safety and Health Convention, 1981), Mkataba Na.187 (Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006) Mkataba Na.167 (Occupational Safety in Construction Convention, 1988), Mkataba Na.161 (Occupational Health Services Convention, 1995), Mkataba Na.176 (Safety and Health in Mines Convention,1995) na Mkataba Na.184 (Safety and Health in Agriculture Convention, 2001);

iii) Kusajili mahali pa kazi **1,847** sawa na asilimia **123** ya sehemu za kazi 1,500 zilizopangwa zilisajiliwa. Mahali pa kazi **137** zilipewa leseni za kukidhi vigezo vya Sheria namba 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi rejea Kiambatisho Na. 5); na

iv) Mafunzo na kozi mbalimbali kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi yamefanyika kwa maafisa **1,700** wa afya na usalama mahali pa kazi kutoka sekta mbalimbali. Kozi hizi zinajumuisha kozi ya Taifa ya Usalama na Afya *(National Occupational Safety and Health Course (NOSHC))*, Utoaji wa Huduma ya Kwanza Makazini *(industrial first aid),* Usalama katika Kufanya kazi za Juu (safety in working at height), na namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi. Aidha, OSHA iliandaa mikutano **6** na wamiliki wa viwanda mbalimbali na semina moja kwa Kamati **2** za Kudumu za Bunge kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi rejea Kiambatisho Na. 6).

**Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA)**

**49.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) imetekeleza kazi zifuatazo:

i) Kusajili watafutakazi **1,249** na kuunganisha watafutakazi **503** kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi na kutoa mafunzo elekezi kwa watafutakazi 584 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa jinsi ya kuweza kuajiriwa;

ii) Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania **1,116** nje ya nchi ikiwemo Oman **918**, Dubai **164,** India **21**, Ujerumani **6**, Japani **5** na Qatar **2**;

iii) Kutoa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na soko la ajira kwa wahitimu watarajiwa 665 kupitia Taasisi 2 za elimu ya juu ambazo ni Mwalimu Nyerere Memorial Academy na Taasisi ya Uhasibu Tanzania;

iv) Kutoa ushauri kwa watafuta kazi **1,157** juu ya uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira (*Vocational Guidance and Employment Counseling*) ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika;

**Shirika la Tija la Taifa (NIP)**

**50.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Shirika la Tija la Taifa (NIP) lina jukumu la kutoa mafunzo mbalimbali, kufanya tafiti zenye lengo la kuinua tija pamoja na kutoa huduma ya ushauri ili kuinua tija sehemu za kazi nchini. Katika mwaka 2014/2015, Shirika liliendesha mafunzo **48** ya kuinua tija mahali pa kazi na mafunzo ya kujenga uwezo sawa na asilimia **60** ya lengo lililopangwa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki **820** kutoka taasisi mbalimbali. Pia NIP ilifanya tafiti moja sawa na asilimia **25** ya lengo na kutoa huduma ya ushauri katika kukuza tija kwa mteja mmoja.

**Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) imetekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya kaguzi **kumi na sita** (16) za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria zilizounda Mifuko hiyo na pia Sheria ya Mamlaka, Kanuni na Miongozo yake kama inafuatwa ipasavyo. Kati ya hizo, kaguzi **tano** (5) zilifanyika eneo la kazi (onsite inspection) na kumi na mbili (12) zilifanyika kwa njia ya taarifa (offsite inspection);

ii) Kutoa elimu kwa watu **1,700,000** kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) na Makampuni binafsi. Aidha, elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa katika njia mbalimbali ikiwemo, Makala ya magazeti **102**, vipindi **13** vya televisheni, vipindi **326** vya redio na mitandao mingine ya digitali **20**, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika maonesho;

iii) Kufanya tafiti **mbili (2)** zenye lengo la kupanua wigo wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Hizi zilijumuisha huduma zisizo rasmi za bima ya afya (social health insurance) na misaada ya kijamii (social assistance);

iv) Kutoa Kanuni mpya ya kuwianisha mafao ya pensheni (pension benefits harmonization rules) iliyoanza kutumika tarehe 01 Julai, 2014; Kanuni hizi zimewezesha mafao ya pensheni kuongezeka kutoka **67%** kwenda **72.5%,** kuthaminisha penshen (indexation) na kutumia wastan wa mshahara wa miaka **3** badala ya miaka **5;**

v) Kusajili Mifuko **miwili (2)** ya hiyari na kutoa miongozo na kanuni za utendaji wao wa kila siku;

vi) Kusimamia na kufanikisha zoezi la kuhuisha michango (reconciliation of contributions) ya wanachama wa vyuo vikuu pamoja na mashirika ya umma yaliyokuwa na matatizo. Vyuo **11** na mashirika **35** yalifanyiwa kazi, ambapo kiasi cha shillingi **1,104,319,525** kilihuishwa;

vii) Kupokea na kutatua malalamiko mbalimbali ya wanachama, ambapo kati ya malalmiko **509** yaliyopokelewa, malalamiko **501** yalifanyiwa kazi na kutatuliwa;

viii) Kufanya marekebisho ya muongozo wa kujumuisha vipindi vya uchangiaji ili kuwezesha wanachama waliochangia mfuko zaidi ya mmoja kujumlisha vipindi vyake vifikie kigezo cha kupata pensheni; Muongozo huu utasaidia wanachama zaidi ya **11,070** ambao waliathirika na muundo wa kuchangia zaidi ya Mfuko mmoja wa lazima, wakati wa utumishi wao;

ix) Kuandaa Mfumo hadhari wa kusimamia na kukagua Mifuko na watoa huduma (Risk Based Supervision Framework);

x) Kutengeza mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kutoa taarifa kati ya Mifuko na Mamlaka (Electronic Submission Portal); na

xi) Kufanya tathmini ya Mifuko yote ya pensheni kwa kushirikiana na shirika la Kazi duniani (ILO) kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Mifuko, kuanda fao la wasio na ajira (unemployment benefit). Pia, tathmini hii inaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza idadi ya Mifuko ya pensheni iliyopo.

**Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limetekeleza kazi zifuatazo:-

i) Limekusanya mapato ya kiasi cha shilingi milioni **629,404.4** sawa na asilimia **60.3** ya lengo na kutumika katika kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza

katika vitega uchumi, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 7**);

ii) Limeendesha semina **3,066** kwa waajiri na wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii;

iii) Shirika limeandikisha wanachama wapya **113,517** ambao ni asilimia **24.5** ya lengo lililokusudiwa ambapo wanachama **37,144** ni kutoka katika sekta isiyo rasmi (Informal Sector), vikundi vya akiba ya kuweka na kukopa (SACCOS) na Vikoba;

iv) Mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi milioni **239,658.4** yalilipwa ambazo ni sawa na asilimia **145.2** ya lengo la kulipa shilingi milioni **164,999.7.** Jumla ya wanachama waliolipwa mafao ni **65,932**;

v) Katika kuboresha Huduma kwa Wateja wake; Shirika limepata Cheti cha Kimataifa cha Utoaji Huduma Bora Kwa Wateja (***ISO 90001: 2008 Certification***). Aidha Shirika limekamilisha Mpango wa Biashara Endelevu (*Business Continuity Plan*) na pia limeweza kuunganisha Ofisi zake zote za Mikoa na Wilaya katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa (*Fibre Cabe*), Shirika liko katika hatua za mwisho za maandalizi ya mpango wake wa kupima afya za baadhi ya wanachama wake (*Preventive Health Checks*) na kufanya Mkutano Mkuu wa Nne wa wadau wa NSSF mwezi Mei 2015;

vi) Shirika limeshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii (Corporate Social Responsibility) katika maeneo yafuatayo: Mchango kusaidia shughuli za kijamii katika jimbo la Mwabara (Nuru ya Maendeleo ya Jinsia), udhamini michezo ya Ramadhan Bonanza (*Union sports Club*), udhamini wa mkutano wa kila mwaka wa TAPSEA, kusaidia Mwenge wa uhuru Kilwa (DAS Kilwa), udhamini wa mchezo wa mpira wa miguu (*Mwidau Foundation*), Udhamini mkutano mkuu wa mwaka (*Tanzania Editors Forum*), mchango wa kuendesha kambi ya waogeleaji (Champion rise swim club), kusaidia mkutano mkuu wa mwaka ma mkutano wa kisayansi (*Tanzania Surgical Association*), Mchango kusaidia Iftar ya wabunge (Ngurdoto Mountain Lodge), Ulinzi na Uhifadhi wa Mazingira (DAS Kilwa), udhamini wa gharama za Traksuti **100** Mwenge Pangani, Udhamini wa gharama za kila mwaka za mikutano ya kisayansi (*Tanzania Dental Association),* (*sponsoring africa corporate governance network meeting*), kusaidia watoto wa mitaani (*Retention home upanga*) na Rukwa, msaada kwa Taasisi ya maendeleo kwa viziwi Tanzania, Kampeni ya kuongeza muamko wa utunzaji wa mazingira, kusaidia wasiojiweza, kusaidia Mkapa HIV/AIDS Foundation, kuchimba visima ukerewe, udhamini wa mwanamke na uchumi campaign, udhamini wa rock city marathon, kusaidia mchango ya makazi ya nyumba za wazee, usaidizi kwa SOS children village, mchango kusaidia ununuzi wa "Patient monitor" (Muhimbili), Mchango kwa ajili ya kuondoa

umaskini (*Kisesa Development Fund*), *Rufiji Social Development*, Mkapa Fellows Program, pia michango kwa Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Bagamoyo, *Zanzibar legal Services* na shughuli zinginezo nyingi ambazo ni kwa manufaa ya jamii nzima kwa ujumla;

vii) Shirika limeendelea na utaratibu wa kutoa mikopo katika sekta isiyo rasmi (Informal Sector), kwa wanachama wake katika vikundi vya SACCOS na VICOBA ambapo **shilingi bilioni 51.80** zimetolewa kwa wanachama **6,506** katika Wilaya zifuatazo: Temeke, Ilala, Kinondoni, Arumeru Mashariki, Singida Mjini, Kigoma Vijijini, Masasi na Karagwe. Shirika linatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, mtumie fursa hii kuwafahamisha watu wajiunge na NSSF ili wapate mikopo;

viii) Shirika linaendelea na Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao unatarajiwa kukamilika Disemba 2015;

ix) Shirika limekamilisha miradi ya ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro na Wilaya ya Ilala kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Aidha, Shirika limeendelea na ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi mkoani Shinyanga, hoteli ya kisasa katika mkoa wa Mwanza ambao umefikia asilimia **30** na kuendelea na ujenzi wa jengo la Mzizima, Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu Farm) - nyumba mchanganyiko na ujenzi wa nyumba za bei nafuu Mtoni Kijichi awamu ya tatu ambao unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2015/2016;

x) Katika miradi inayofanywa kwa ushirikiano na Wadau wengine (*Joint Venture Projects*); miradi ya ujenzi wa Hospitali ya "Clinic" ya Apollo jijini Dar es Salaam na ujenzi wa ofisi za RITA (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency*) itakamilika mwaka wa Fedha 2014/2015; Ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (*MP's Village*), mtaalamu/mwelekezi anakamilisha kuandaa michoro. Aidha, Shirika linasubiri udhamini kutoka Serikali ili kuanza Miradi ya Jengo la Maadili. Na pia katika ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Serikali Nchi nzima, Kampuni ya Watumishi "*Housing Limited*" inasubiriwa kukamilisha taratibu, ili Shirika liweze kushiriki; na

*xi)* Shirika limeendelea na uthaminishaji mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 300 katika eneo la Mkuranga, taratibu za ununuzi na taratibu za kupata Washauri Elekezi *(Cosultantants)* wa mradi huu zinaendelea.

## III. TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

**53.** ***Mheshimiwa spika,*** kama ambavyo nimeshaeleza katika aya zilizotangulia, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration)* ni

Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara yangu yenye jukumu la kusuluhisha migogoro ya kikazi, kuamua migogoro ya kikazi na kuratibu shughuli za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*). Vile vile Tume ina jukumu la kutoa elimu ya kuzuia migogoro mahali pa kazi.

**54.** ***Mheshimiwa spika*****,** katika mwaka 2014/15, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (**Fungu15**) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **4,531,723,550** kati ya fedha hizo shilingi **1,824,223,550** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na shilingi **2,707,500,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, **Shilingi 982,966,133.84** sawa na **asilimia 54** ya fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na **shilingi 668,047,148.16** sawa na **asilimia 25** ya fedha za Matumizi mengine (OC ) zilitolewa na kutumika na Tume.

**Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu na Kazi ya Tume kwa Mwaka 2014/15:**

**55.** ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2014/15, Tume imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

ii) Migogoro **11,435** ilipokelewa na kusajiliwa hadi tarehe 30/04/2015. Jumla ya migogoro **4,141** ilishughulikiwa na kumalizika sawa na asilimia **36.** Migogoro 2,657 ilisuluhishwa sawa na asilimia **23** na migogoro **1,484** ilitolewa uamuzi sawa na asilimia **13**. Migogoro **7,294** sawa na asilimia **64** inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali za uamuzi;

iii) Kuwezesha Kamati ya Huduma Muhimu kutembelea na kuifanyia uchunguzi kampuni ya Songas ambapo Kamati ilibaini kuwa Kampuni hiyo ina sifa ya kuwa sekta inayotoa Huduma Muhimu; na

iv) Taasisi **35** zilipewa mafunzo kuhusu dhana ya ushirikishwaji wa wafanyakazi, matumizi sahihi ya Sheria za Kazi, wajibu wa wajumbe katika Baraza na namna bora ya kutatua migogoro ya kikazi.

## D. MPANGO WA KAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### I. WIZARA YA KAZI NA AJIRA

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia Sheria na Viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija

kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Utekelezaji kwa mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

**Usimamizi Kazi na Huduma za Ukaguzi**

i) Kufanya jumla ya kaguzi **4,800** katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waajiri wanaokiuka sheria;

ii) Kuboresha upangaji wa kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kwa kuunda Bodi moja ya mishahara;

iii) Kuimarisha majadiliano ya utatu kwa kujenga uwezo wa Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (***LESCO***) na Wajumbe wa Bodi ya mishahara ikiwa ni pamoja na kuwezesha vikao vyake;

iv) Kuimarisha na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na utumikishwaji wa watoto (*National Action Plan on Elimination of Child Labour)* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wabia wa maendeleo;

v) Kufanya uelimishaji kwa wadau na umma kwa ujumla kuhusu Sheria za Kazi;

vi) Kuhamasisha majadiliano ya pamoja kati ya waajiri na wafanyakazi pamoja na vyama vyao kwa lengo la kuboresha maslahi ya wafanyakazi, hatimaye kuongeza tija na uzalishaji;

vii) Kuimarisha utekelezaji wa Kanuni ya Utatu ya masuala ya UKIMWI katika sehemu za kazi (*Tripartite HIV and AIDS Code of Conduct at Workplaces*) kwa lengo la kupambana na maambukizi na athari zake; na

viii) Kujenga uwezo wa Maafisa Kazi kuhusu mbinu za kisasa za kaguzi na usimamizi wa kazi ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa mashtaka mahakamani.

**Hifadhi ya Jamii**

**57. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuimarisha masuala ya hifadhi ya Jamii ambapo itaanzisha Idara mpya ya Hifadhi ya Jamii itakayokuwa na jukumu la kuratibu masuala yote ya huduma za hifadhi ya jamii kwa lengo la kuendelea kuziboiresha, kupanua wigo na kuzifanya kuwa endelevu. Kazi zitakazotekelezwa katika eneo hili ni zifuatazo:

i) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii nchini;

ii) Kuandaa kanuni za Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Na.20 ya mwaka 2008;

iii) Kuwezesha utendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi,

iv) Kushughulikia tatizo la wanachama kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kabla ya umri wa kustaafu;

v) Kuandaa Kanuni za Baraza la Rufaa la Hifadhi ya Jamii na kuwezesha utekelezaji wa majumuku Baraza hilo; na

vi) Kuridhia Mkataba Na. 102 wa Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO).

**Ukuzaji wa Ajira Nchini**

***58. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu itaendelea kuratibu shughuli za kukuza ajira nchini; ambapo jumla ya ajira **500,000** zinategemewa kuzalishwa katika mwaka 2015/2016 kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Taasisi za Umma, kupitia Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana, Programu ya Kukuza Ujuzi pamoja na uwekezaji katika Sekta Binafsi.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kukuza ajira na kazi za staha nchini, katika mwaka 2015/2016, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kuratibu uhuishaji wa masuala ya ukuzaji ajira kwenye mipango na programu za maendeleo za Halmashauri za Wilaya/Manispaa/Jiji kwenye mikoa 5, Mashirika ya Umma 6 na Wizara/Idara/Wakala za Serikali 5;

ii) Kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali za ujasiriamali; kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji; na Kutenga maeneo maalum ya uzalishaji na kufanyia biashara;

iii) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na Sera ya Tija, Mapato na Bei;

iv) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la ajira nchini,

v) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi wa Nguvukazi (***Skill Development Program)*** chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa - BRN ambapo utekelezaji utahusu (a) Vijana 4,200 kupatiwa mafunzo ya vitendo kazini (intership/Apprenticeship katika sekta sita (maji, nishati &

madini, kilimo, elimu, afya na utalii), (b) Waajiri kuwezeshwa kutoa mafunzo ya ujuzi na ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi 10,000 na (c) Vijana 5,000 wa sekta isiyo rasmi wasio na vyeti vya ujuzi, kupatiwa mafunzo kuwawezesha kupatiwa vyeti vya ujuzi huo;

vi) Kuratibu maonesho ya 16 ya Afrika Mashariki ya Nguvu Kazi/Jua Kali yatakayofanyika Dar es salaam mwezi Desemba 2015;

vii) Kufanya Utafiti wa Hali ya Rasilimali Watu Nchini (Manpower Survey);

viii) Kusimamia utoaji wa huduma za ajira zinazotolewa na Mawakala wa Huduma za Ajira nchini;

ix) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Wakuu wa Mikoa kuhusu ukuzaji wa ajira kwa vijana.

**Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea na jukumu la kusajili na kusimamia vyama vya waajiri na wafanyakazi nchini kama ifuatavyo:

i) Kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya Wafanyakazi na Wajiri na Mashirikisho;

ii) Kufanya kaguzi za vyama ikiwa ni pamoja na kuhakiki taarifa za fedha za vyama;

iii) Kuwaelimisha viongozi wa vyama na wadau wake juu ya wajibu wa vyama na namna ya kushughulikia masuala mbalimbali kwa mujibu wa Sheria za Kazi na Kanuni zake;

iv) Kushughulikia migogoro ya vyama inayojitokeza; na

v) Kushughulikia kesi mahakamani zinazotokana na maamuzi ya Msajili na masuala yanayohusu katiba za vyama.

**Kujenga Uwezo wa Wizara**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kujenga uwezo wa Wizara kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kuwajengea uwezo watumishi **hamsini** (50) wa wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wengine **kumi** (10) kuwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali;

ii) Kuimarisha mahusiano kazini kwa kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi na kushiriki katika matamasha ya michezo;

iii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua nyenzo na vitendea kazi pamoja na kushirikisha Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi;

iv) Kuendelea kutoka mafunzo ya Utawala Bora, Maadili, Vita dhidi ya rushwa mahali pa kazi na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa watumishi **150** wa Wizara kulingana na Sheria na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi watano (5) wanaoishi na virusi vya UKIMWI;

v) Kufanya vikao vinne vya Kamati ya Ajira ya Wizara (mara moja kila Robo ya Mwaka) kwa kuajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo watumishi wenye sifa za Kimuundo na utendaji mzuri wa kazi;

vi) Kuimarisha Ofisi za Kazi za Mikoa ili ziweze kusimamia viwango vya kazi kwa mujibu wa Sheria;

vii) Kuratibu na kusimamia ujazaji wa fomu za OPRAS na utekelezaji wake kwa watumishi **262** wa Wizara;

viii) Kujibu Hoja za Ukaguzi, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa Taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC);

ix) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN);

x) Kuendelea kufuatilia mwenendo wa bajeti kwa kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi;

xi) Kuandaa Mafunzo juu ya sheria Mpya ya Manunuzi kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wizara pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo;

xii) Kuendelea kuelimisha umma juu ya shughuli mbalimbali za Wizara kupitia vyombo mbali mbali vya habari pamoja kuunganisha mtandao wa Mawasiliano wa Wizara na Mkonga wa mawasiliano wa Taifa; na

xiii) Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia kesi zinazohusu Wizara.

## II. TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

**62. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

### Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

**63. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya ukaguzi **20,000** wa kawaida na ukaguzi **21,000** maalum kuhusu afya na usalama mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi **65,000** katika sehemu mbalimbali za kazi;

ii) Kusajili sehemu **3,000** mpya za kazi ili ziweze kukidhi viwango na kanuni za Afya na Usalama Mahali pa Kazi pamoja na kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya chini ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (*The Occupational Health and Safety Act, 2003*);

iii) Kuendelea kutoa mafunzo na kozi mbalimbali za Afya na Usalama Mahali pa Kazi ambapo mafunzo hayo yatajumuisha kozi ya Taifa ya usalama na afya (*NOSHC*), kozi ya utoaji wa huduma ya kwanza makazini (*industrial first aid*), kozi ya usalama katika kufanya kazi za juu (*safety in working at height*), na kozi ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi. Wafanyakazi na Waajiri **3,000** wanatarajiwa kupata mafunzo haya.

iv) Kuanzisha mifumo mbalimbali ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi, mfumo wa kutunza kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa fedha na mfumo wa usimamizi wa vifaa (*Asset tracking system*);

v) Kuendelea kuelimisha wafanyabiashara wadogo na wa kati pamoja na sekta isiyo rasmi ili waweze kuboresha mazingira yao ya kazi kwa kuendesha

warsha, semina na makongamano mbalimbali katika mikoa ya Tanzania Bara;

vi) Kukamilisha uandaaji wa rasimu za kanuni tatu ambapo kanuni mbili ni kuhusu gesi *“Occupational health and safety (Oil and Gas) rules*”, na “(Vessel under pressure regulations na kanuni moja kuhusu utoaji taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi “*Recording and reporting of occupational diseases, injuries and dangerous occurrences rules”*; na

vii) Kushiriki katika taratibu za kuridhia mikataba **sita (6)** ya Kimataifa (ILO Conventions) inayohusiana na Usalama na afya mahali pa kazi. Mikataba hiyo ni Mkataba Na. I55 (*Occupational Safety and Health Convention, 1981*), Mkataba Na.187 (*Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006*) Mkataba Na.167 (*Occupational Safety in Construction Convention, 1988*), Mkataba Na.161 (*Occupational Health Services Convention, 1985)*, Mkataba Na.176 (*Safety and Health in Mines Convention, 1995)* and Mkataba Na.184 (*Safety and Health in Agriculture Convention, 2001).*

**Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA)**

**64. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) umepanga kufanya yafuatayo:-

i) Kushiriki katika zoezi la kutoa mafunzo ya ujuzi (Internship Program) kwa watafutakazi **4,200** ili kuwajengea uwezo wa kushindania fursa katika soko la ajira;

ii) Kusajili watafutakazi **3,000** na kuunganisha watafutakazi **1,000** kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi;

iii) Kutembelea waajiri **1,000** kwa lengo la kubaini idadi na aina ya fursa za ajira;

iv) Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania **1,000** nje ya nchi;

v) Kuendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza Taarifa za Soko la Ajira;

vi) Kutoa mafunzo elekezi (Job search workshops) kwa watafutakazi **1,500** na kutembelea Taasisi **20** za elimu ya juu kwa lengo la kutoa

mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na ushindani wa soko la ajira kwa wahitimu watarajiwa; na

vii) Kutoa ushauri wa kitaalam (*consultancy services*) kwa wadau juu ya masuala ya huduma za ajira hapa nchini.

**Shirika la Tija la Taifa (NIP)**

**65. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara kupitia Shirika la Tija la Taifa (NIP) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika kuongeza Tija sehemu za kazi:

i) Kuendesha mafunzo **80** ya uongozi yatakayohudhuriwa na watumishi **1,200** kutoka taasisi za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (NGO's);

ii) Kutoa huduma za ushauri elekezi kwa wateja **30** katika sekta za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (NGO's);

iii) Kufanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija;

iv) Kuanzisha mahusiano na kushirikiana na taasisi nyingine za tija duniani; na

v) Kuanzisha mahusiano na kushirikiana na wadau wa maendeleo (Development Partners) na taasisi za kimataifa (International Agencies) kwenye huduma za mafunzo, utafiti na ushauri elekezi.

**Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

**66. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) itaendelea kutekeleza hatua za kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kukamilisha tathmini ya Mifuko yote inayofanywa kwa kushirikiana na ILO

ii) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa elimu kwa umma kwa lengo la kuongeza uelewa wa masuala ya hifadhi ya jamii. Elimu hiyo itafanyika zaidi kikanda, ambapo zaidi ya wanachama 2,000,000 wataelimishwa na wanafunzi 100,000 wa vyuo vikuu wataelimishwa. Aidha, Mamlaka itaendelea kutumia Runinga, Redio na Magazeti kuwafikia wananchi wengi zaidi nchi nzima;

iii) Kuendelea na zoezi la ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria na kwa manufaa ya wanachama wake ambao ndio msingi wa kuanzishwa kwao.

Kaguzi 29 zitafanyika, 5 zikiwa ni za eneo la kazi (onsite supervision) na 24 zikiwa si za eneo la kazi (offsite surveillance);

iv) Kufanya tafiti tano (5) katika maeneo ya ubora wa huduma, mafao mbadala kwa sekta isiyo rasmi na bima za afya ya jamii. Kutokana na tafiti hizi Mamlaka itabuni program na mafao maalum ya hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo rasmi mijini na vijijini;

v) Kutekeleza mageuzi katika sekta ya hifadhi ya jamii yaliyoainishwa katika Mpango wa Mageuzi ya Sekta hiyo katika kipindi cha 2012-19.

vi) Kuendelea na kazi ya usajili wa Mifuko ya hiyari 4 (Supplementary Schemes), Mameneja Wawekezaji 2 (Fund Managers) na Watunza nyaraka (Custodians) na kutoa miongozo na kanuni za utendaji wao wa kila siku; na

vii) Kuboresha Mfumo wa usimamizi unaotumia vipimo vya hathari (Risk Based Supervision) kwa kuandaa miongozo.

**Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

**67.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2015/16 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii litatekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kukusanya jumla ya Shilingi milioni **1,561,032.15** na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo;

ii) Kuimarisha uandikishaji na ukusanyaji michango ya Wanachama katika sekta isiyo rasmi (*informal sectors*), kuendelea na ukusanyaji wa madeni kwa waajiri na pango kwa wapangaji wa majengo ya NSSF;

iii) Kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii;

iv) Shirika litaendelea na mpango wa kupima afya za wanachama wake (*Preventive Health checks*);

v) Kufanya mkutano mkuu wa tano wa wadau wa NSSF;

vi) Kukamilisha tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao;

vii) Kukamilisha ujenzi wa daraja la Kigamboni mwezi Desemba, 2015;

viii) Kuendelea na ujenzi wa vitega uchumi; Hospitali ya Apollo, Mradi wa nyumba za bei nafuu mia nane Mtoni Kijichi awamu ya Tatu, Ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (*Tuangoma na Dungu Farm*), ujenzi wa kijiji cha kisasa Kigamboni (*Azimio Satellite town*), ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma ( MP's Village) na Ofisi za Bunge Dar es Salaam na Tanga (*Commercial Complex*), kituo cha kimataifa cha Magari Mwandiga Kigoma, Ujenzi wa Majengo ya NSSF/Maadili, NSSF/TBC; na

ix) Kuanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya ofisi Makao Makuu katika Mkoa wa Dar es Salaam, ofisi katika Wilaya za Kinondoni, Temeke, Tarime na Kasulu, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, wilaya za Temeke na Kinondoni. Pia kuanza ujenzi wa kituo cha michezo (*Sports Academy*).

## III. TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

**68.** ***Mheshimiwa spika*,** naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16. Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

i) Kusuluhisha na kuamua migogoro **15,000** ya kikazi na kuandaa taarifa;

ii) Kufanya tafiti juu ya migogoro ambayo haijasajiriwa katika Tume na kuishughulikia;

iii) Kuendesha mafunzo **200** ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya kuzuia na kutatua migogoro mahali pa kazi;

iv) Kuandaa na kusimamia vikao vya Makamishna wa Tume na vikao vya Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*);

v) Kuandaa na kusambaza juzuu ya tatu ya kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Vol. 3*.) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kwa matumizi ya wadau wa Tume;

vi) Kuwezesha uanzishwaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi;

vii) Kupokea na kusajili mikataba ya kuunda mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi;

viii) Kufanya tathmini ya hali ya ushirikishwaji Tanzania Bara;

ix) Kujenga uwezo wa Tume kwa kuwaendeleza watumishi kitaaluma; na

x) Kuendeleza mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

## E. SHUKRANI

**69.** ***Mheshimiwa spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2014/2015 yametokana na ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa **Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga (Mb),** Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa Jimbo la Segerea kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu **Bwana Eric Shitindi** pamoja na Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa njia ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii *(LESCO)*, Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*) kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo.

***71.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa maendeleo ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yangu. Hivyo, napenda shukrani zangu za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO), UNDP, UNICEF, UNFPA, Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark (DANIDA), Idara ya Kazi ya Marekani, Serikali ya Brazil na Benki ya Dunia (WB).

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ndani ya Bunge na nje ya Bunge inayolenga kuboresha utendaji katika Wizara yangu.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba niishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Albert Obama, Mbunge wa Manjovu kwa kuendelea kuisimamia vyema Wizara yangu. Wizara itaendelea kutekeleza ushauri na maelekezo ya Kamati kwani yanalenga kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wangu wa Mara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa upendo wao na mchango mkubwa ninaoupata.

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **38,883,129,000** kwa Wizara ya Kazi na Ajira (**Fungu 65**) na jumla ya Shilingi **4,097,054,000** kwa Tume ya Ushuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii katika mchanganuo ufuatao:-

**(a) Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira**

i) Shilingi **4,158,089,000** zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara;

ii) Shilingi **14,725,040,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC);

iii) Shilingi **20,000,000,000** zitatumika katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**(b) Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

i) Shilingi **1,910,043,000** zitatumika kulipa mishahara ya watumishi wa Tume; na

ii) Shilingi **2,187,011,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC).

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa anwani: www.kazi.go.tz

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| ATE | - | Association of Tanzania Employers |
| CMA | - | Commission for Mediation and Arbitration |
| EAC | - | East African Community |
| ILO | - | International Labour Organization |
| LESCO | - | Labour, Economic and Social Council |
| NGOs | - | Non Governmental Organizations |
| NIP | - | National Institute for Productivity |
| NSSF | - | National Social Security Fund |
| OSHA | - | Occupation, Safety and Health Agency |
| PROSPER | - | Promoting Sustainable Practices to Eradicate Child Labour |
| RITA | - | Registration, Insolvency and Trusteeship Agency |
| SSRA | - | Social Security Regulatory Authority |
| TaESA | - | Tanzania Employment Services Agency |
| TUCTA | - | Trade Unions Congress of Tanzania |
| UKIMWI | - | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| WCF | - | Workers Compensation Fund |

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1**

# AJIRA ZILIZOZALISHWA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 10 YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE

| SEKTA KUU | SEKTA NDOGO | KIPINDI CHA KWANZA CHA MIAKA MITANO | | | | | | KIPINDI CHA PILI CHA MIAKA MITANO | | | | | IDADI YA AJIRA KIPINDI CHA MIAKA 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2006/07** | **2007/08** | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **JUMLA** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** | **2014/15** | **JUMLA** | |
| AJIRA SERIKALINI | Elimu | 13,359 | 17,470 | 19,525 | 23,636 | 28,774 | **102,763** | 29,258 | 43,362 | 36,073 | 36,071 | **144,764** | **247,527** |
| | Afya | 2,717 | 3,553 | 3,971 | 4,807 | 5,852 | **20,901** | 5,951 | 8,820 | 11,221 | 3,452 | **29,444** | **50,345** |
| | Sekta nyingine | 1,406 | 1,839 | 2,055 | 2,488 | 3,029 | **10,818** | 3,080 | 4,565 | 2,321 | 5,274 | **15,240** | **26,058** |
| | **JUMLA NDOGO** | **17,483** | **22,862** | **25,552** | **30,931** | **37,655** | **134,483** | **38,289** | **56,747** | **49,615** | **44,797** | **189,448** | **323,931** |
| MIRADI YA MAENDELEO YA SERIKALI | Kilimo | 38,531 | 50,387 | 56,314 | 68,170 | 82,990 | **296,392** | 9,017 | 122,980 | 130,974 | 154,560 | **417,531** | **713,923** |
| | Miundombinu | 18,501 | 24,194 | 27,040 | 32,733 | 39,849 | **142,317** | 59,792 | 1,033 | 32,132 | 107,527 | **200,484** | **342,801** |
| | Nishati | 136 | 178 | 199 | 241 | 294 | **1,050** | 268 | 380 | 453 | 378 | **1,479** | **2,529** |
| | Miradi ya kijamii | 9,500 | 12,424 | 13,885 | 16,808 | 20,462 | **73,079** | 34,561 | 50,246 | 8,686 | 9,455 | **102,948** | **176,027** |
| | **JUMLA NDOGO** | **66,669** | **87,182** | **97,439** | **117,953** | **143,595** | **512,838** | **103,638** | **174,639** | **172,245** | **271,920** | **722,442** | **1,235,280** |
| SEKTA BINAFSI | Viwanda Vidogo na Kati | 2,408 | 3,149 | 3,520 | 4,261 | 5,187 | **18,526** | 9,946 | 2,436 | 7,192 | 6,524 | **26,098** | **44,624** |
| | Uwekezaji kupitia EPZ | 6,243 | 8,163 | 9,124 | 11,045 | 13,446 | **48,020** | 15,100 | 9,254 | 26,381 | 16,911 | **67,646** | **115,666** |
| | Uwekezaji kupitia TIC | 30,049 | 39,295 | 43,918 | 53,164 | 64,722 | **231,148** | 82,834 | 59,010 | 149,594 | 34,184 | **325,622** | **556,770** |
| | Mawasiliano | 16,983 | 22,208 | 24,821 | 30,046 | 36,578 | **130,637** | 76,900 | 86,702 | 13,619 | 6,809 | **184,030** | **314,667** |
| | Sekta nyingine | 38,265 | 50,039 | 55,926 | 67,700 | 82,417 | **294,348** | 1,184 | 8,603 | 211,970 | 192,895 | **414,652** | **709,000** |
| | **JUMLA NDOGO** | **93,948** | **122,855** | **137,309** | **166,216** | **202,350** | **722,679** | **185,964** | **166,005** | **408,756** | **257,323** | **1,018,048** | **1,740,727** |
| **JUMLA YA AJIRA ZILIZOZALISHWA KISEKTA** | | **178,100** | **232,900** | **260,300** | **315,100** | **383,600** | **1,370,000** | **327,891** | **397,391** | **630,616** | **574,040** | **1,929,938** | **3,299,938** |

***Chanzo: Wizara ya Kazi na Ajira***

**Kiambatisho Na. 2**

## ORODHA YA VYAMA VILIVYOSAJILIWA TANZANIA BARA KUANZIA MWAKA 2000 HADI 2015

### (a) VYAMA VYA WAFANYAKAZI:

| Na. | Jina la Mwanachama | Namba ya Usajili | Tarehe ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 1. | Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers Union (TUICO) | 001 | 11/9/2000 |
| 2. | Tanzania Plantation and Agriculture Workers Union (TPAWU) | 002 | 11/9/2000 |
| 3. | Communication and Transport Workers Union of Tanzania (COTWU)(T) | 003 | 11/9/2000 |
| 4. | Tanzania Teachers Union TTU (CWT) | 004 | 13/9/2000 |
| 5. | Tanzania Mines Energy, Construction and Allied workers union (TAMICO) | 005 | 13/9/2000 |
| 6. | Tanzania Railways Workers Union (TRAWU) | 006 | 13/9/2000 |
| 7. | Tanzania Fishing and Maritime Workers Union (TAFIMU) | 007 | 13/9/2000 |
| 8. | Tanzania Seafarers Union (TASU) | 008 | 15/9/2000 |
| 9. | Researchers, Academicians AND Allied WORKERS UNION (RAAWU) | 009 | 15/9/2000 |
| 10. | Tanzania Local Government Workers Union (TALGWU) | 010 | 15/9/2000 |
| 11. | Conservation, Hotels, Domestic and Allied Workers Union (CHODAWU) | 011 | 15/9/2000 |
| 12. | Tanzania Union of Government and Health Employees Union (TUGHE) | 012 | 22/9/2000 |
| 13. | Industrial and General Workers Union of Tanzania (IGWUTA) | 013 | 8/6/2001 |
| 14. | Tanzania Social Services Industry Workers Union (TASIWU) | 014 | 8/6/2001 |
| 15. | Tanzania Union Journalists (TUJ)* | 015 | 8/6/2001 |
| 16. | Dock Workers Union of Tanzania (DOWUTA) | 016 | 17/6/2002 |
| 17. | Tanzania Union of Private Security Employees (TUPSE) | 017 | 5/11/2004 |
| 18. | Telecommunication Workers Union of Tanzania (TEWUTA) | 018 | 24/11/2004 |
| 19. | Tanzania Media Workers UNION (TMW – UNION)** | 019 | 8/5/2006 |
| 20. | Tanzania Pilot's UNION (TPU) ** | 020 | 10/8/2006 |

| Na. | Jina la Mwanachama | Namba ya Usajili | Tarehe ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 21. | Tanzania AGROFORESTRY WORKERS UNION (TAWU)** | 021 | 7/8/2006 |
| 22. | Mufindi Paper Employees Trade Union (MPETU) | 022 | 16/10/2008 |
| 23. | The Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union (THTU) | 023 | 12/12/2008 |
| 24. | Financial, Industrial, Banking, Utilities, Commercial and Agro processing Industries Trade Union (FIBUCA) | 024 | 24/7/2009 |
| 25. | Tanzania Road Transport Workers Union (TARWOTU) | 025 | 21/1/2013 |
| 26. | Tanzania Medical Dental and Pharmaceutical Workers Union (TMDPWU) | 026 | 28/1/2013 |
| 27. | Printing Publishing and Packaging Workers Union of Tanzania (PRIPPAWUTA) | 027 | 31/1/2013 |
| 28 | Domestic Social Services Hospitality Industry and Tourism Workers Union (DOSHITWU) | 028 | 21/1/2013 |
| 29. | National Union of Mine and Energy Workers of Tanzania (NUMET) | 029 | 20/2/2013 |
| 30 | TAZARA Workers Union-Tanzania(TAWUTA) | 030 | 20.09.2013 |
| 31 | Chama Cha Kutete Haki Na Maslahi ya Waalimu Tanzania (CHAKAMWATA) | 031 | 18/3/2015 |

***Chanzo:*** ***Kitengo cha usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri – Wizara ya Kazi na Ajira***

**NB:** *** Kimefutwa kutokana na ukiukwaji wa Sheria**
****Maombi ya kuvifuta yamewasilishwa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi**

**(b) VYAMA VYA WAAJIRI**:

| Na | Jina la Mwanachama | Namba ya Usajili | Tarehe ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 1. | Association of Tanzania Employers (ATE) | E1 | 14/11/2003 |
| 2. | Tanzania Association of Agriculture, Commerce, Industry and Mining Employers (TAACIME)* | E2 | 12/12/2008 |

***Chanzo:*** ***Kitengo cha Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri – Wizara ya Kazi na Ajira***

**(c) MASHIRIKISHO:**

| Na | Jina la Mwanachama | Namba ya Usajili | Tarehe ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 1. | Trade Unions Congress of Tanzania (TUCTA) | FED.01 | 18/5/2001 |
| 2. | East African Trade Union Confederation (EATUC) | CONF.1 | 9/10/2008 |
| 3. | East African Employers Organization (EAEO) | E.3 | 12/9/2011 |
| 4. | Federation of East African Teacher's Union | FED. 02 | 25/11/2013 |

***Chanzo:*** ***Kitengo cha Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri – Wizara ya Kazi na Ajira***

**Kiambatisho Na. 3**

**AJIRA ZILIZOZALISHWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2014 HADI MEI, 2015**

| Aina ya Mradi/Sekta | Sekta ndogo | Idadi ya ajira |
|---|---|---|
| Ajira Serikalini | Elimu | 36,071 |
| | Afya | 3,452 |
| | Sekta nyingine | 5,274 |
| | **Jumla ndogo** | **44,797** |
| Miradi ya Maendeleo ya Serikali | Kilimo | 154,560 |
| | Miundombinu | 107,527 |
| | Nishati | 378 |
| | Miradi ya Kijamii | 9,455 |
| | **Jumla ndogo** | **271,920** |
| Sekta Binafsi | Viwanda Vidogo na Kati | 6,524 |
| | Uwekezaji kupitia EPZ | 16,911 |
| | Uwekezaji kupitia TIC | 34,184 |
| | Mawasiliano | 6,809 |
| | Sekta nyingine | 192,895 |
| | **Jumla ndogo** | **257,323** |
| **Jumla Kuu** | | **574,040** |

***Chanzo:*** ***Idara ya Ajira – Wizara ya Kazi na Ajira***

**Kiambatisho Na. 4**

**MAOMBI YALIYOPEKELEWA NA VIBALI VILIVYOTOLEWA VYA AJIRA ZA WAGENI KUFANYA KAZI KATIKA SEKTA MBALIMBALI KIPINDI CHA JULAI, 2014 HADI APRILI, 2015**

| Sekta | Mapendekezo ya Maombi | | |
|---|---|---|---|
| | Yaliyokubaliwa | Yaliyokataliwa | Jumla |
| Ujenzi | 2,102 | 86 | 2,188 |
| Biashara | 1,697 | 80 | 1,777 |
| Uzalishaji viwandani | 1,613 | 76 | 1,689 |

| Sekta | Mapendekezo ya Maombi | | |
|---|---|---|---|
| | **Yaliyokubaliwa** | **Yaliyokataliwa** | **Jumla** |
| Madini | 405 | 14 | 419 |
| Usafirishaji na Uhifadhi | 344 | 13 | 357 |
| Elimu | 311 | 14 | 325 |
| Utalii | 289 | 13 | 302 |
| Utafiti na Bodi za Kitaalamu | 294 | 10 | 304 |
| Hoteli | 284 | 13 | 297 |
| Habari na Mawasiliano | 190 | 8 | 198 |
| Afya | 152 | 5 | 157 |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 147 | 6 | 153 |
| Uzalishaji wa Maji, Umeme na Gesi | 128 | 3 | 131 |
| Fedha na Bima | 125 | 5 | 130 |
| Mashirika yasiyo ya Kiserikari na Mashrika ya Kimataifa | 116 | 3 | 119 |
| Maendeleo ya Makazi | 106 | 3 | 109 |
| Uchezaji Kamari na Michezo ya Kubahatisha | 99 | 8 | 107 |
| Utoaji wa Mizigo Bandarini | 98 | 4 | 102 |
| Utengenezaji Magari | 85 | 2 | 87 |
| Uchapaji | 77 | 3 | 80 |
| Ulinzi | 42 | 1 | 43 |
| Usambazaji wa Maji, Umeme na Gesi | 18 | 1 | 19 |
| Huduma za Kiutawala | 12 | 0 | 12 |
| Huduma nyingine | 153 | 12 | 165 |
| **JUMLA** | **8,890** | **381** | **9,271** |

***Chanzo: Idara ya Ajira – Wizara ya Kazi na Ajira***

**Jedwali Na: 5**

**IDADI YA MAHALI PA KAZI PALIPOSAJILIWA NA KUPEWA LESENI BAADA YA KUKIDHI VIGEZO VYA SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI**

| KANDA | MKOA | USAJILI SEHEMU ZA KAZI |
|---|---|---|
| **Ukanda wa Pwani** | Dar Es Salaam | 901 |
| | Pwani | 40 |
| | Morogoro | 107 |
| **Ukanda wa Kusini** | Lindi | 29 |
| | Mtwara | 84 |

| KANDA | MKOA | USAJILI SEHEMU ZA KAZI |
|---|---|---|
| | Ruvuma | 42 |
| **Ukanda wa Kaskazini** | Arusha | 70 |
| | Kilimanjaro | 59 |
| | Manyara | 7 |
| | Tanga | 49 |
| | Mwanza | 124 |
| | Kagera | 43 |
| | Mara | 41 |
| **Ukanda wa Ziwa Victoria** | Shinyanga | 30 |
| | Simiyu | 7 |
| | Geita | 17 |
| | Mbeya | 71 |
| | Rukwa | 5 |
| **Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini** | Iringa | 26 |
| | Njombe | 12 |
| | Katavi | 1 |
| | Dodoma | 35 |
| | Singida | 19 |
| **Ukanda wa Kati** | Tabora | 19 |
| | Kigoma | 9 |
| **JUMLA** | | 1,847 |

Chanzo: Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi

**Jedwali Na: 6**

**JEDWALI KUONYESHA IDADI YA WAFANYAKAZI NA WAAJIRI WALIOPEWA MAFUNZO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015**

| Na | AINA YA KOZI | Julai 2014-Machi 2015 |
|---|---|---|
| **1** | Kozi ya Taifa | 48 |
| **2** | Kozi ya namna ya Kuunda na Kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi | 326 |
| **3** | Kozi ya Utoaji wa Huduma ya Kwanza Makazini | 1,115 |
| **4** | Kozi ya Kutathmini vihatarishi vya Afya na Usalama | 50 |
| **5** | Kozi ya Usalama katika kufanya kazi za juu | 43 |
| **6** | Kozi ya uelewa wa masuala ya Afya na Usalama kwa wahitimu wa Chuo Kikuu cha Muhimbili | 18 |
| **JUMLA** | | **1,700** |

Chanzo: Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi

**Kiambatisho Na. 7**

## MALENGO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2014/2015 & 2015/16

## MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA

(Tshs 000,000)

| Na. | MATUMIZI | LENGO LA 2014/15 | LENGO LA JULAI-MAR. | MATUMIZI HALISI JULAI-MAR. | UTEKELEZAJI (%) | LENGO LA 2015/16 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Malipo ya Mafao | 219,999.8 | 164,999.7 | 239,658.4 | 145.2 | 231,140.99 |
| 2 | Matumizi ya Uendeshaji | 118,128.4 | 98,933.2 | 79,954.7 | 80.8 | 133,179.89 |
| 3 | Matumizi ya Maendeleo | 19,943.4 | 19,943.2 | 9,891.0 | 49.6 | 25,938.82 |
| 4 | Vitega Uchumi | 1,079,545.3 | 760,036.4 | 299,900.2 | 39.5 | 1,170,772.4 |
| **JUMLA** | | **1,437,616.9** | **1,043,912.5** | **629,404.3** | **60.3** | **1,561,032.15** |

Chanzo: Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)



Waziri wa Kazi na Ajira Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Bwana Guy Ryider wakitoka katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere Mjini Dar es salaam baada ya kumalizika kwa Kongamano la Kukuza Ajira kwa Vijana lililofanyika mwezi Desemba 2013.